Pasaka na Biblia
(Easter and the Bible)

na

Ellis P. Forsman

Pasaka na Biblia

na

Ellis P. Forsman

Octoba 7, 2011

Pasaka na Biblia

Mdo. 12:4

"Pasaka inachukuliwa kama sikukuu kuu ya Wakristo." Inasheherekewa na mamilioni ya watu kila mwaka. Pia inaeleweka kama "sikukuu kubwa nay a zamani katika kalenda ya Wakristo."

Kinachoifanya ionekane "siku takatifu" ni kwamba watu huishirekea kwa ukumbusho wa ufufuo wa Kristo. Matokeo yake watu wengi miongoni mwa Wakristo huandamana kusherekea pasaka kidini.

Sehemu nyingi za ibada hutumia siku ya juma pili kama siku pekee ya kufanya maigizo na muziki wakiwa wamesimamia katika ufufuo wa Kristo. Hakika, wengi huichukulia kuwa ni mbaya – na ikiwezekana ni upotofu – kwa kanisa ya Kikristo WASIPO sherekea Pasaka kidini.

Vilevile, Pasaka ni dini iliyotungwa na mwanadamu; haikuanzishwa na Yesu Kristo au mitume wake.

Katika somo hili tutaangalia katika:

- Matokeo ya kihistoria na matendo yaliyofanyika ya Pasaka.
- Biblia inazungumziaje Pasaka.
- Hitimisho la mtu binafsi na kusanyiko.

Historia kuhusu pasaka

Pasaka ilipotokea:

Neno Pasaka limetoholewa kutoka kwenye neno Saxon "*Pasakra*: mungu mwanamke wa chemchemi, ambaye katika kumtii dhabihu zilitolewa kuhusu wakati wa Pasaka kila mwaka. Kwenye karne ya 8 mtu aitwaye Anglo Saxon alianzisha jina hili ili kusheherekea ufufuo wa Kristo." (Kamusi ya Biblia ya Anger).

Pasaka (*Gr. Pascha*) Pasaka, na hivyo ikatafsiriwa katika kila kifungu cha maandiko isipokuwa Mdo. 12:4. (kamusi ya Biblia ya Anger).

"Ilivyotafasiriwa 'Pasaka' katika Mdo. 12:4. …neno Pasaka halitokani na Ukristo…(hai) kuanzishwa na Kristo. …(hili lilikuwa) jaribio la kuiga sherehe za kipagani kuzileta katika Ukristo." (Kamusi ya Vine's).

Mageuzi ya Pasaka yaliyofanyika:

Mapema kama kwenye karne ya nane, neno "Pasaka" lilitumika kuelezea sherehe za Kikristo ya ufufuo wa Kristo.

Hisitoria ya kidunia inasema kulikuwa na muingiliano kati ya Wapagani na Wakristo katika karne ya 2. Historia ya kidunia inasema Ukristo ulijaribu kuwavutia ulimwengu wa wapagani kwa mkanganyiko wa kufufuka kwa Kristo kwa sherehe za kipagani.

Katika karne 4 kanisa la Catholiki (kupitia Constantine, maliki wa Kirumi) aliendeleza mazingira tofauti yaliyozunguka Pasaka: kiufundi, kama ni lini inapaswa kusherekewa.

Hataivyo, historia inasaidia, haishindwi na ni sawa na historia ya Biblia.

Inachosema Biblia kuhusu "Pasaka"

Ikiwa na tendo lolote kama ya kanisa: mamlaka lazima yaanzishwe kwa yote tunayofanya.

Kol. 3:17, "*Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*"

Kama nguzo na msingi wa kweli, kanisa la Bwana linatii kichwa chaake:

1 Tim. 3:15, "*Lakini nikikawia kuja upate kujua jinsi iwapasavyo kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo, na msingi wa kweli.*"

Yesu Kristo ni kichwa cha kanisa.

- Efe. 5:23-24, "*Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili.*

Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo."

- Efe. 5:32, "*Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa.*"
- Wakristo – wanaounda mwili wa Kristo (Kanisa lake) – hawadhanii mapenzi ya Mungu.

1 Kor. 2:9-11, "*Lakini kama ilivyoandikwa, mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Rogo huchunguza yote hata mambo ya Mungu. Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu.*"

Wakristo wanapaswa tu kuabudu katika roho na kweli.

Yoh. 4:23-24, "*Lakini saa inakuja nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Rogo nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*"

Hivyo, wale walioko katika mwili wa Kristo wafanye mambo yote kulingana na mafundisho yake.

2 Yoh. 1:9, "*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.*"

Wakati pekee neno "Pasaka" inatumika katika toleo la Mfalme Yakobo la 1611.

Mdo. 12:4, "*Alipokwisha kumkamata, akamweka gerezaani akamtia mikononi mwa vikosi vinne vya askari wanne wanne, wamlinde, akitaka baada ya Pasaka kumtoa na kumweka mbele ya watu.*"

Neno la Kiyunani "pascha" halijulikani kama ni tafsiri inayopotosha. Hakujawahi kutokea tafsiri yenye upuzi au kutokuwa na furaha kuliko (Albert Barnes).

Tafsiri sahihi ya "pascha" ni "Pasaka." (ile ya Kiyahudi). Hii ilikuwa ni sherehe ya Kiyahudi, kulingana na sheria ya Agano la Kale.

Kutoka 12:12-14, "*Maana nitapita kati ya nchi ya Misri usiku huo, nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa mwanadamu na wa mnyama; nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri, Mimi ndimi BWANA. Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazo kuwamo, nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu lisiwapate pigo lolote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri. Na siku hii itakuwa ukumbusho kwenu, nanyi mtaifanya iwe sikukuu kwa BWANA; mtaifanya iwe sikukuu katika vizazi vyenu vyote, kwa amri ya milele.*"

Mdo. 12:4, (au andiko lolote la Agano Jipya) HAIONGELEI pasaka kama tendo la Agano Jipya linalofaanywa na Wakristo katika karne ya kwanza.

Biblia ya NIV ya Mdo. 12:4, "*Alipokwisha kumkamata, akamweka gerezaani akamtia mikononi mwa vikosi vinne vya askari wanne wanne, wamlinde, akitaka baada ya Pasaka kumtoa na kumweka mbele ya watu.*"

Kwa sababu Biblia imenyamaza kuhusu kuisherekea itakuwa makosa kwa kanisa kufanya tendo hilo la kidini.

Muhimu zaidi: sisi kama Wakristo tunapaswa kumwabudu Mungu katika Roho na kweli.

Kwa vile maandiko ya Agano Jipya imenyamaza kuhusu Pasaka, kanisa ambalo ni la Bwana halisherekei/ kutenda tendo kama la sikukuu ya kidini.

Hitimisho

Wakati Pasaka ni maarufu na inakusudiwa vyema kama sikukuu ya kufufuka kwake Kristo katika ulimwengu wa dini, hataivyo, Mungu, amenyamaza kabisa kuhusu siku hii.

Kama Wakristo, hamu yetu ni kumtumikia Bwana kwa imani – kwa neno lake lililofunuliwa amelinyamazia jambo hili – hivyo hakujuimuisha sikukuu hii.

Tunasherekea mauti ya Kristo na kufufuka kwake kila siku ya kwanza ya juma, sio mara moja kwa mwaka